Cambridge Assessment International Education

# Cambridge IGCSE™

**SWAHILI** **0262/02**

Paper 2 Listening **June 2023**

TRANSCRIPT **Approximately 45 minutes**

This document has **8** pages. Any blank pages are indicated.

© UCLES 2023

Eng: Cambridge Assessment International Education
Cambridge IGCSE Examination in Swahili
Paper 2 Listening, May/June 2023
Turn over now.

*(Pause 5 seconds)*

TLR: **Zoezi 1**

TLR: Utasikia vipande vinane vifupi vilivyorekodiwa.
Jibu maswali 1–8 katika nafasi uliyopewa.
Majibu yako yawe mafupi iwezekanavyo.
Utasikia kila rekodi mara mbili.

TLR: Swali 1

M: * Mdogo wangu anayeitwa Salama ameanza shule leo. Alikuwa na furaha wiki nzima huku akihadithia kwamba atakaa juu ya dawati na kutumia kalamu yake kuandikia. Mimi nilimwambia ingebidi ajitayarishe kulia kwani mtu aliyezoea kuwa naye kutwa, mama, hataingia naye darasani. Yeye alicheka na kusema yeye si kilizi. Siku ilipowadia, kweli aligoma kuingia shule peke yake. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 2

F: * Mgahawa mpya umefunguliwa mtaani kwetu. Juzi nilienda kula chakula cha mchana. Nilitaka kunywa juisi ya maembe na mtindi lakini hakukuwa na maembe, kwa hivyo nilikunywa ya nanasi. Mwenye mgahawa alitueleza kwamba yeye hununua mahitaji yake yote kutoka sokoni ambapo wakulima huuza bidhaa zao wenyewe kwa hivyo mapishi yake hutegemea msimu wa vyakula. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 3

M: * Nimeshaamua nitakachosoma nifikapo chuo kikuu. Mwanzoni nilitaka kusoma lugha ya Kifaransa, halafu nikaona bora kusoma Kireno. Lakini, ingawa lugha hizo zinazungumzwa sehemu tofauti za bara la Afrika, ni lugha ambazo hazina asili ya Kiafrika. Hivyo basi nimeamua kusoma Kiswahili. Kazi niliyonayo sasa ni kutafuta chuo kikuu cha kusomea. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 4

F: * Mji wa Mbeya ni mahali pazuri kwa kutembelea wakati wa likizo. Kuna vijiji vingi vilivyozungukwa na mashamba makubwa ya michai. Pia kuna mimea mingi tofauti ya matunda na vyakula kama miparachichi. Cha ajabu ni kuwa wengi hupenda kurudi Mbeya kwa sababu ya ukarimu wa wenyeji. Je umewahi kuenda huko? **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 5

M: * Je utafanya nini wakati wa likizo yako ya mwezi wa saba? Kama bado huna mpango, tafadhali jitolee mara mbili kwa wiki ili kuwasaidia watoto yatima wanaoishi katika nyumba ya mayatima iliyopo nje ya mji. Nyumba hiyo ina watoto ambao wanahitaji msaada wa kufundishwa kusoma na kuandika. Kwa kujitolea utaweza kuwapa ujuzi ambao utawasaidia maishani mwao. Asanteni kwa kuwasiliana nasi. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 6

F: * Nilipanda meli kutoka Dar es Salaam hadi Unguja. Njiani bahari ilikuwa na mawimbi makubwa yaliyoifanya meli yetu itikisike sana. Msukosuko huo ulinifanya nishindwe kumeza chochote. Nilipofika Unguja, nilitafuta mgahawa wa kula. Niliona mgahawa mzuri barabarani lakini kila chakula walichokuwa nacho kilikuwa na nyama hivyo nilishindwa kula kwani mimi sili nyama. Safari nyingine nitabeba chakula kutoka nyumbani, itakuwa bora zaidi kwangu. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 7

M: * Je Sia, utasafiri kuenda Lamu mwisho wa mwaka?

F: Ndiyo. Nimefurahi sana. Nilishindwa kuenda mwaka uliopita kwa sababu ya mlipuko wa homa ya matumbo.

M: Ugonjwa bado upo, kwa nini huogopi kusafiri?

F: Ingawa ni kawaida yangu kuwa msafi kwa kunawa mikono ili kujikinga na magonjwa yanayoambukizwa. Nimepata nguvu ya kusafiri baada ya kuchanjwa wiki mbili zilizopita. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 8

F: * Juma, ulisahau kuniambia tamasha la sauti za busara kule Unguja lilikuwaje mwaka huu.

M: Eh kweli. Nilisahau. Tamasha lilikuwa kubwa kama kawaida. Watu walikuwa wengi, nilifurahia akiba yangu ya fedha iliyonisaidia kukutana na watu kutoka dunia nzima. Niliimba na kucheza dansa kwa siku mbili mfululizo. Pia nilihudhuria shughuli zote zilizoandaliwa. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 1. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 2. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 2.

*(Pause 30 seconds.)*

© UCLES 2023

TLR: **Zoezi 2**

TLR: Utamsikia msichana anazungumza kuhusu nzige Afrika Mashariki.
Msikilize na malizia sentensi.
Andika neno moja au maneno mawili tu katika kila nafasi.
Utasikia rekodi mara mbili.

F: * Kuna sehemu nyingi za Afrika Mashariki ambazo zimepata mlipuko mkubwa wa nzige mwaka huu ambao umeleta uhaba wa chakula kwani wadudu hao wameharibu mazao mengi shambani.

Nzige wana uwezo wa kusafiri kwa umbali wa kilomita 150 kila siku. Wao husafiri kwa kasi sana na kuathiri sehemu tofauti za nchi. Wao pia hula chakula kingi kwa siku kwani husafiri katika makundi makubwa yanayokula mno. Mwishoni mwa mwaka uliopita kulikuwa na mvua nyingi sana iliyoleta nzige wengi. Nzige hutaga mayai zaidi ya 120 kila mara na huishi kwa muda wa miezi mitatu hadi mitano lakini watu hufikiri wao hufa baada ya wiki mbili tu. Hivi sasa nzige wamekuwa wengi hadi kufikia kiwango cha kuwa janga huku Afrika Mashariki.

Kampuni moja iitwayo Wadudu ni Lishe yenye makao yake makuu nchini Rwanda imeanza kubadili mawazo ya watu kuhusu nzige. Badala ya kuwaangalia tu na kusikitika, kampuni hii imejaribu kugeuza tatizo la nzige kuwa biashara kwa kuwalipa wakulima wanaokamata nzige mashambani. Ingawa karne za hofu kuhusu nzige si rahisi kubadilika.

Kawaida pale kampuni hii inapogundua kundi la nzige linawasili, huitangazia jamii husika kuwa wananunua nzige. Kampuni hugawa mifuko ya kuwafungia nzige pamoja na makaratasi ya kuwakamatia ambayo ni makubwa, meusi na ya plastiki. Wafanyakazi wa kampuni huwafundisha watu kukamata nzige wakati wa usiku, ambapo wadudu wanapumzika.

Hivyo wakulima wanaweza kutikisa tu mimea na nzige wenyewe wanadondoka kutoka mitini na kuokotwa kirahisi. Nzige wanaokamatwa huchanganywa kwenye chakula cha mifugo ili kukifanya kiwe na protini nyingi. Lengo la baadaye la kampuni ni kuwawezesha watu kukamata nzige kabla ya wadudu hao kusababisha uharibifu. Jambo hilo linaweza kuwa njia nzuri sana ya kudhibiti nzige. **

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: Sasa sikiliza tena.

*(Pause 3 seconds. Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 2. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 3. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 3.

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: **Zoezi 3**

TLR: Utawasikia watu sita wakizungumza kuhusu mashindano ya michezo shuleni.

Oanisha wasemaji na mawazo katika orodha A–G. Kwa kila msemaji, andika herufi (A–G) katika mstari wa jibu.

Tumia kila herufi mara moja tu. Kuna herufi ya ziada isiyohitajika.

Utasikia rekodi mara mbili.

TLR: * Msimulizi 1

M: Sitasahau siku yangu ya kwanza kushiriki kwenye mashindano ya michezo kati ya shule tofauti mkoani kwetu. Siku mbili kabla ya mashindano, mvua kubwa ilinyesha kwa hivyo tope lilitapakaa. Mimi nilikuwa mshiriki wa mbio. Muda wangu wa kukimbia ulipofika, niliteleza na kuangukia uso. Watu walicheka. Nilifahamu kwamba, kama ningepata hasira, ningeshindwa kushindana. Nikaamua kufanya kama sikuwasikia. Huwezi kuamini, nilisimama huku nimejaa tope, nikakimbia na kushinda.

TLR: Msimulizi 2

F: Jambo ambalo ninachukia wakati wa mashindano ya michezo ni shughuli za usafi ambazo tulilazimika kufanya ili shule yetu ipendeze. Shule yetu ilikuwa katikati ya mji na ilikuwa na uwanja mzuri sana wa michezo kwa hivyo mashindano yote yalifanyika kwetu. Uwanja ulikuwa na nyasi nzuri na hata pale mvua iliponyesha, hakukuwa na tope la kuwachafua watu. Kwa kawaida mimi nilicheza mpira wa kikapu na nilikuwa hodari sana.

TLR: Msimulizi 3

M: Wiki chache kabla ya mashindano ya michezo kati ya shule, ratiba ya masomo hubadilika na walimu hutumia muda mwingi kuzungumzia mashindano. Zamani nilicheza katika timu ya shule ya mpira wa kikapu lakini sikupenda sana kwani ilibidi kukimbia kwa hatua ndefu zilizonichosha. Hivi sasa moyo wangu upo kwenye mpira wa miguu. Tuchezapo wenzetu hutufurahia kwa kupiga kelele na miluzi.

TLR: Msimulizi 4

F: Siku za mashindano ya michezo shuleni sisi sote hukusanyika katika shule moja iliyopo katikati ya mji. Kwa kawaida sisi hupanda basi la shule asubuhi na mapema na huwa na shamra shamra safarini. Nimeanza kushiriki nilipokuwa mdogo na hivi sasa nimekuwa nahodha wa timu ya shule yetu. Jambo nilipendalo sana ni kurudi shuleni kwetu na kombe la ushindi ambalo hupambwa ofisini kwa mwalimu mkuu ili watu wote walione. Unaposhindana lengo ni moja tu – kushinda.

TLR: Msimulizi 5

M: Raha kubwa ya kuenda kwenye mashindano ya michezo ya shule ni kukutana na wanafunzi wa shule tofauti. Kuna watu ambao wanaenda kwenye mashindano ili kupata medali na kombe kwa kujionyesha. Mimi ninadhani muhimu kuliko vyote ni kushiriki katika mashindano. Nilipoenda mwaka jana niliunda mahusiano mengi. Nina hamu ya kuenda tena mwaka huu kuwaona wote tena.

TLR: Msimulizi 6

F: Unapojenga urafiki na wanafunzi ambao unashindana nao basi hutaweza kushindana vizuri. Rafiki zako wawe wanafunzi wenzako wa kutoka shuleni kwako tu. Wale unaokutana nao kwenye mashindano hawakusaidii chochote. Kusafisha uwanja wa mazoezi utafanya na wenzako kutoka shule moja. Fahari ya kombe utaihisi na wenzako wa shule moja. Hilo ni muhimu kukumbuka. Mimi huenda kwenye mashindano kutazama tu. Sivutiwi na vyeo vizito kama unahodha wa timu. Labda nitakapoenda shule ya sekondari nitaweza kufanya hivyo. **

*(Pause 5 seconds.)*

TLR: Sasa sikiliza tena.

(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 3. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 4. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 4.

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: **Zoezi 4**

TLR: Utasikia mazungumzo kati ya Jakson na Zakiya.

Sikiliza mazungumzo hayo na soma maswali.

Kwa kila swali chagua jibu sahihi kati ya A, B au C.

Weka alama ya tiki kwenye kisanduku sahihi.

Utasikia rekodi mara mbili.

F: * Vipi mambo Jakson. Uliniambia utanisimulia kile kisa cha wavuvi waliotajirika kule Yemen.

M: Eh ndiyo kweli. Yaani habari yao imenisisimua sana. Inasemekana kulikuwa na kundi la wavuvi baharini huko Yemen. Basi, mara wakamwona nyangumi anaelea baharini. Si jambo la ajabu kukuta samaki wakielea, kwa hivyo wao wakampita.

F: Alaa, enhe ...

M: Lakini mara, mmoja wao ambaye hivi karibuni amehamia kwenye eneo hilo akawaambia wamrudie. Yeye alitoka mji mwingine unaoitwa Hodeida. Akawafahamisha kwamba yule nyangumi alikuwa anatoa harufu mbaya ambayo yeye anaitambua kuwa ni madini adimu. Aliwaambia kwamba kule kwao Hodeida nyangumi hutapika kilo nne au tano hivi za hayo madini na wangeweza kupata pesa.

F: Sasa ikawaje?

M: Basi akawabembeleza wale wavuvi wenzake wamrudie yule nyangumi. Kwa vile alikuwa mkubwa mno, wenzake walihisi usumbufu kurudi. Aliwabembeleza na kuwaahidi jasho lao halitapotea. Mwishoni takriban wavuvi 100 waliokuwa karibu nao walijiunga nao na wakayapata hayo madini.

F: Wana bahati!

M: Ndiyo! Unajua hayo madini huota tu yenyewe kwenye tumbo la nyangumi. Kawaida nyangumi huyatapika hayo madini yeye mwenyewe ingawa wengine hawafanyi hivyo. Hayo madini yanaitwa ambagrisi na siku hizi hutumiwa kutengeneza manukato. Zamani yalitumiwa kama dawa na pia kama aina ya kiungo kwenye chakula. Ni madini adimu sana. Hayapatikani kirahisi.

F: Lakini mbona ulisema yana harufu mbaya sana?

M: Ndiyo. Lakini wataalamu wenyewe huchukua hayo madini na kuyapeleka kwenye maabara. Huko mafuta maalumu hutolewa kutoka kwenye hayo madini. Mafuta hayo hufanya manukato yanukie kwa muda mrefu zaidi na yawe ghali sana. Tunaweza kusema madini hayo ni kama almasi iliyo tumboni mwa samaki huyo. Basi wavuvi walipata kilo 127 za madini. Sasa wameshauza hayo madini na wamepata takribani Dola za Kimarekani milioni moja na nusu. Pesa hizo wamegawana na pia wametoa kama msaada kijijini kwao.

F: Na hao wavuvi wamefanyia nini na pesa walizopata?

M: Kwanza, si wavuvi wote waliokuwa na boti za kuvulia samaki. Hapo awali wavuvi zaidi ya kumi wakipanda boti moja kuenda kuvua halafu baada ya kazi waligawana samaki waliowapata. Sasa baada ya kupata hayo madini, maisha yao yamebadilika kabisa. Karibu wote wamejinunulia boti la kuvulia. Wametambua kuwa boti ndiyo kitu kitakachowapa uhuru wa uwezo wa kujiendeleza kiuchumi. Sasa hawatakuwa na haja ya kusubiriana ili kuenda kuvua halafu kugawana wanachovua.

F: Nimeelewa.

M: Unajua, wengi kati ya hao wavuvi walikuwa vijana ambao hawakuoa pale awali kwani hawakuwa na mahari ya kutosha na walikuwa na wasiwasi wa kushindwa kukidhi mahitaji ya familia. Sasa wengi kati yao wameshachumbia wasichana, wataoa na wanategemea kuishi maisha ya kifamilia. Wale ambao walikuwa tayari wana familia, maisha yao yatakuwa bora zaidi. Wavuvi wengi wameamua kujenga nyumba ingawa hawajali kuhusu magari, baisikeli na televisheni. Jambo la muhimu walilolifanya ni kwamba hawajaacha kuvua. Hebu niambie, wewe ungefanya nini kama ungekuwa mmojawapo kati ya hao wavuvi?

F: Mimi ningesafiri duniani kote! Ningetumia pesa zote kuona dunia na watu tofauti wanavyoishi. Wewe je?

M: Mimi ningewekeza kwenye biashara halafu ningetengeneza pesa zaidi. Kama ningalikuwa mvuvi, ningenunua boti kama nne au tano, ningeajiri wavuvi wengine na kukuza biashara yangu ya uvuvi. Nisingekuwa na boti moja tu, ningetaka biashara kubwa sana. Jambo la kusafiri ili kuiona dunia lingekuwa jambo la mwisho kabisa kwangu. Kwanza nahisi kusafiri kuona dunia ni kupoteza muda na pesa. Jambo muhimu ni kujijenga mimi mwenyewe ili nizidi kuwa tajiri.

F: Wewe unapenda zaidi kuwa na vitu, mimi ninapenda zaidi kuifurahisha roho yangu.

M: Nina uhakika kuwa roho yangu ingefurahi sana tu kama ingeona kuwa nimekuwa tajiri. **

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: Sasa sikiliza tena.

(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 4, na mwisho wa mtihani.

Eng: That is the end of the examination.

© UCLES 2023

**BLANK PAGE**

Permission to reproduce items where third-party owned material protected by copyright is included has been sought and cleared where possible. Every reasonable effort has been made by the publisher (UCLES) to trace copyright holders, but if any items requiring clearance have unwittingly been included, the publisher will be pleased to make amends at the earliest possible opportunity.

To avoid the issue of disclosure of answer-related information to candidates, all copyright acknowledgements are reproduced online in the Cambridge Assessment International Education Copyright Acknowledgements Booklet. This is produced for each series of examinations and is freely available to download at www.cambridgeinternational.org after the live examination series.

Cambridge Assessment International Education is part of Cambridge Assessment. Cambridge Assessment is the brand name of the University of Cambridge Local Examinations Syndicate (UCLES), which is a department of the University of Cambridge.